# TAARIFA YA DAWA ZA KULEVYA YA MWAKA 2019/2020

## 1.0 MADHUMUNI

**Mheshimiwa Spika,**

Taarifa hii inatolewa mbele yako na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kulingana na matakwa ya Kifungu cha 8 cha Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya Nam. 9/2009. Taarifa hii ina lengo la kuonesha hali halisi ya dawa za kulevya ilivyokuwa kwa mwaka 2019 - 2020.

## 2.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,**

Tatizo la Dawa za Kulevya lilikuwepo kwa miaka mingi katika Visiwa vya Zanzibar. Kabla ya mwaka 1964, tatizo hilo lilitokana na matumizi makubwa ya tumbaku, sigara, pombe na bangi. Mara tu baada ya Mapinduzi tatizo hilo lilipungua kutokana na hatua mbali mbali zilizochukuliwa kwa wakati huo. Mnamo mwaka 1980 tatizo la dawa za kulevya liliongezeka tena kwa kasi kubwa kwa kuibuka kwa aina mpya ya dawa za kulevya aina ya kokeni, mandrax na heroin.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na hali hiyo, mwaka 1996 Serikali iliamua kuchukua hatua za kufuatilia na kupinga uingizaji na matumizi ya dawa za kulevya Zanzibar kwa kuanzisha Idara Maalumu ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya iliyokuwa chini ya Ofisi ya Waziri Kiongozi. Ilipofika Novemba mwaka 2000, Idara hiyo ilihamishiwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na kupewa majukumu ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya pamoja na Kinga na Tiba kwa walioathirika na matumizi ya dawa hizo.

**Mheshimiwa Spika,**

Serikali iliendelea kuongeza nguvu katika mapambano kwenye usafirishaji na uingizaji wa dawa za kulevya kwa kupitisha Sheria ya Dawa na Kinga ya Usafirishaji wa Dawa za Kulevya Nam. 16/2003. Kutokana na kuwepo kwa sheria hiyo, mwaka 2004 Serikali ilifanya mabadiliko ya kazi za Idara hiyo na kupewa jukumu pia la kupambana na kurekebisha tabia kwa walioathirika. Idara iliyokuwa ikisimamia

majukumu hayo nayo ikaitwa Idara ya Kupambana na Dawa za Kulevya na Kurekebisha Tabia. Katika utekelezaji wa sheria hiyo, kasoro mbali mbali za udhibiti wa uingizaji, uuzaji na kupambana na dawa za kulevya zilibainika na kupelekea kutungwa kwa sheria mpya ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya Nam. 9/2009 ili kuimarisha mapambano zaidi. Sheria hii ndio inayotumika hadi sasa na ndio sheria iliyoanzisha Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**

Taarifa hii imegawika katika sehemu kuu sita zinazoelezea historia ya Tume na Sheria ya Dawa za Kulevya, tatizo la dawa za kulevya juhudi za Serikali katika kudhibiti usafirishaji wa dawa za kulevya na katika kudhibiti matumizi ya dawa za kulevya. Aidha, taarifa inaelezea inaelezea hali ya ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa katika kudhibiti dawa za kulevya sambamba na mafanikio, changamoto na hatua za baadae.

## 3.0 MANTIKI

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na Dawa za Kulevya na Uhalifu Duniani (UNODC - 2020) inakadiriwa kuwa zaidi ya watu robo bilioni (milioni 271/5.5%) wenye umri wa miaka 15-64 duniani kote wanatumia Dawa za Kulevya. Kati ya hao, watu Milioni 35 (13%) wanakabiliwa na tatizo la utegemezi na watu milioni 11.3 (0.23%) wanatumia dawa kwa njia ya kujidunga sindano.

**Mheshimiwa Spika,**

Utafiti uliofanywa na Kitengo Shirikishi cha UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma (ZIHTLP - 2019) unasema kuwa hapa Zanzibar watu 2,200 wanatumia dawa za kulevya kwa njia za kujidunga sindano wakiwemo wanawake na wanaume ambapo vijana wa kiume wameonekana kuathirika zaidi. Wapo ambao wameathirika kwa kupata maradhi mbalimbali yakiwemo magonjwa ya mapafu, akili, moyo, shindikizo la damu, homa ya Ini B na C pamoja na maambukizi ya VVU na UKIMWI. Wapo pia walioathirika kwa kutengwa na jamii pamoja na kuhatarisha

usalama kwa jamii kwa kufanya vitendo vya kihalifu ikiwemo wizi, uporaji, ubakaji na uharibifu wa mali na miundombinu.

**Mheshimiwa Spika,**

Pamoja na juhudi zinazoendelea kuchukuliwa za udhibiti usambazaji wa dawa za kulevya hapa nchini, bado kuna ongezezo kubwa la kesi za dawa za kulevya. Mwaka 2012 tulikuwa na kesi 237 wakati mwaka 2020 tuna kesi 454. Mwaka 2017 ulishuhudiwa kuwa na ongezeko la kutisha la kesi 694. Kwa ukubwa wa nchi yetu, kuwa na kesi 694 ndani ya mwaka mmoja si jambo la kulifumbia macho.

## 4.0 MAPITIO YA TAARIFA YA HALI YA DAWA ZA KULEVYA 2019 - 2020

### 4.1 Hali ya Usafirishaji na Usambazaji wa Dawa za Kulevya

**Mheshimiwa Spika,**

Taarifa inaonesha kuwa nchi za ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini zinasadikiwa kuwa ni miongoni mwa njia zinazotumika kupitishia dawa za kulevya kwenda sehemu mbalimbali duniani. Taarifa za Kipolisi zimeonesha kuwa katika kipindi cha 2012-2020 jumla ya watuhumiwa 3,810 wakiwemo wanaume 3,577 na wanawake 233 wamekamatwa nchini kwa tuhuma za kujihusisha na uhalifu wa dawa za kulevya ambapo jumla ya kilo 51.5 za heroini, kilo 2,946 za bangi, kilo 5.4 za valiamu na kilo 19.71 za kokeni zilikamatwa. Vile vile, jaduweli namba 2.2.1 linaonesha kuwa mwenendo wa kesi za dawa za kulevya umeongezeka baina ya 2016 – 2018 na kupungua kidogo kasi yake baada ya hapo. Hata hivyo hii haimaanishi kwamba wanaojihusisha na uhalifu wa dawa za kulevya wamepungua, bali inaweza pia kuwa na maana ya usimamizi usio imara kwa kesi za aina hiyo. Taarifa inaonesha kuwa kati ya kesi zote zilizokamatwa mwaka 2016, 30% zilifungwa polisi na kesi 26% zilifungwa Mahkamani; Mwaka 2017 wastani wa 50% zilikwama katika upelelezi, 13% zilifungwa polisi na 4% zilifungwa mahakamani (rejea jaduweli nam 2)**.**

## 4.2 Matumizi ya Dawa za Kulevya

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mujibu wa utafiti wa mwaka 2010 uliofanywa na UNODC, inakadiriwa kuwa watu 7,000 mpaka 10,000 wanatumia Dawa za Kulevya Zanzibar. Sababu mbalimbali zimetajwa kupelekea matumizi ya dawa za kulevya zikiwemo shindikizo rika, kuiga, malezi mabaya, binaadamu kutokuwa na uwezo wa kujikwamua na matatizo anayokabiliana nayo na kuwa na marafiki wenye tabia mbaya.

**Mheshimiwa Spika,**

Matokeo ya matumizi ya dawa za kulevya ni maradhi na hivyo Mamlaka za Serikali na jamii kwa ujumla zinawajibika kushughulikia tiba na marekebisho ya tabia kwa waathirika na vile vile kuondoa mazingira hatarishi ili kuzuia vijana wapya kujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya. Katika kuhakikisha hilo, jitihada zimechukuliwa na Selikali kwa kushirikiana na wahusika mbalimbali kuhakikisha upatikanaji wa matibabu na huduma za marekebisho ya tabia zenye lengo la kuwatoa watu katika utegemezi wa dawa za kulevya na kuwarudisha katika jamii kuendelea na ujenzi wa taifa. Hata hivyo, takwimu zilizo katika jaduweli namba 5 zinaonesha kuwa bado kuna hali ya waliopata nafuu kurudi tena katika matumizi ya dawa za kulevya. Ndugu Wajumbe, hali hii inapaswa kujadiliwa kwa kina na hatimaye kuweka mikakati imara zaidi itakayowazuia waliopata nafuu wasirudi katika matumizi ya dawa za kulevya na vile vile kuwakinga wengine wasijiingize katika matumizi ya dawa za kulevya.

## 4.3 Ukamataji wa Dawa za Kulevya

**Mheshimiwa Spika, Ndugu Wajumbe,**

Ukamataji ni moja kati ya jitihada zinazochukuliwa na Serikali katika udhibiti wa Dawa za Kulevya. Katika kipindi cha miaka miwili 2019-2020 kumeripotiwa jumla ya kesi 957 (503 mwaka 2019 na 454 mwaka 2020) katika vituo vya Polisi vya Mikoa yote ya Zanzibar pamoja na Kitengo Maalumu cha Polisi cha Kupambana na Dawa za Kulevya (ADU). Kesi hizo zina jumla ya watuhumiwa 526 ambapo watuhumiwa 514 ni wanaume na 12 ni wanawake. Mkoa wa Mjini Magharibi ndio Mkoa ulioripoti kesi nyingi 291 (30%), ADU iliripoti kesi 201 (21%), Mkoa wa Kusini Unguja kesi

173 (18%), Mkoa wa Kaskazini Unguja ulioripoti kesi 113 (12%), Mkoa wa Kusini Pemba kesi 121 (13%) na kesi kidogo zimeripotiwa katika Mkoa wa Kaskazini Pemba 58 (6%).

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kipindi cha hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2020 jumla ya vyombo 15 vya usafiri (Honda Click na Pikipiki 5 na gari 10) vilivyohusika na uhalifu wa dawa za kulevya vimeshikiliwa na kesi zake zinaendelea Mahakamani kama inavyooneshwa katika jaduweli Nam. 8.

### 4.4 Mafunzo, Mikutano na Vikao.

**Mheshimiwa Spika,**

Serikali imeendeleza juhudi kwa kufanya mikutano, mafunzo na vikao kwa wahusika wa mapambano dhidi ya dawa za kulevya ili kuwajengea uwezo na mbinu mpya katika kupambana na dawa za kulevya. Katika kipindi hicho Serikali iliendesha mafunzo kwa wadau wa madiko katika bandari zisizo rasmi ambapo washiriki kutoka shehia 53 kwa Unguja na Shehia 62 kwa Pemba walipatiwa mafunzo yaliyokuwa na lengo la kuhamasisha jamii kuhusu athari, udhibiti na mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Aidha, elimu imetolewa kwa wanafunzi na walimu wa skuli za Msingi na Sekondari, wanafunzi wa Vyuo Vikuu pamoja na wafanyakazi wa vikosi vya ulinzi na usalama. Jumla ya watu 16,534 Unguja na Pemba walifikiwa katika mpango huo. Tume ya Kudhibiti na Uratibu wa Dawa za Kulevywa iliendesha programu ya kinga ya msingi kwa watoto wa skuli 4 za maandalizi ambazo ni Jang’ombe, Kidutani, Saateni na Magomeni mpango uliohusisha wanafunzi 412 na walimu 9.

### 4.5 Kuziwezesha Programu za Upataji Nafuu.

**Mheshimiwa Spika,**

Serikali imeendelea kutoa mchango katika kuziwezesha programu za upataji nafuu zinazoendeshwa na taasisi binafsi na za kiserikali. Programu hizo ni *nyumba za upataji nafuu* (sober houses), mikutano ya tiba za kifamilia (family therapy) na kuwajengea uwezo watumiaji baada ya kupata nafuu. Katika kipindi cha miaka miwili (2019 – 2020) Serikali imezipatia ruzuku nyumba 8 za upataji nafuu Unguja

na Pemba kwa lengo la kusaidia gharama za uendeshaji ili kuiokoa jamii na janga la matumizi ya dawa za kulevya. Nyumba hizo ni Trent, Detroit, Zanzibar Youth Forum, Free At Last, Tawabina na Nyarugusu kwa Unguja, na kwa upande wa Pemba ni Mkoroshoni (Chake chake) na UMATI (Wete). Jumla ya watumiaji waliopokelewa katika nyumba hizo kwa kipindi hicho ni 750.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kuziwezesha programu za upataji nafuu, Tume ilifanya mikutano saba ya Tiba ya kifamilia (4 Unguja na 3 Pemba). Familia 240 za wazazi/walezi wenye vijana wanaotumia dawa za kulevya na waliopata nafuu zilishiriki katika mikutano hiyo. Lengo la mikutano hiyo ni kuzungumza na wazazi/walezi ili kutoa fursa ya kujadili ili nao wawe chachu ya kuwasaidia na kuwafariji watoto wao badala ya kuwatenga na kunakopelekea kuwazidishia msongo wa mawazo.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kuwajengea uwezo vijana waliopata nafuu, Tume imemdhamini kijana mmoja alieamua kuachana na matumizi ya dawa za kulevya kwenda kusoma masomo ya Utalii (Tourism information) ngazi ya cheti, katika Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA). Aidha, katika kupunguza madhara ya kiafya watumiaji wa dawa za kulevya waliwezeshwa kushiriki mikutano ya ngazi mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa iliyofanyika Arusha, Austria, Kenya, Afrika Kusini na nyenginezo. Jumuiya ya ZANPUD (Zanzibar Network for People who Used Drugs) imekuwa wajumbe katika *East African Harm Reduction na African PUD*, na kupitia taasisi hiyo Zanzibar imepata nafasi ya uwenyekiti wa *East African Harm Reduction.*

**Mheshimiwa Spika,**

Serikali inaendelea na ujenzi wa Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia kwa vijana walioathirika na matumizi ya dawa za kulevya ili kuwatibu vijana hao. Kituo hicho kinategemea kuanza kutoa huduma katika mwaka wa fedha 2021/2022.

## 4.6 Ushirikiano na Taasisi za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa

**Mheshimiwa Spika,**

4.6.1 Tume imekuwa na ushirikiano na taasisi mbalimbali za ndani ya nchi vikiwemo vyombo vya ulinzi na usalama, taasisi zinazoshughulika na usafiri na usafirishaji, pamoja na asasi za kiraia za Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

4.6.2 Kumekuwa na mashirikiano na mashirika mbalimbali ya kikanda na kimataifa likiwemo Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na Dawa za Kulevya na Uhalifu Duniani (UNODC). Aidha, kumekuwa na mazungumzo na taasisi mbalimbali ikiwemo Taasisi inayoshughulikia mapambano dhidi ya Dawa za Kulevya ya Marekani (Drug Enforcement Administration) na Shirika la "UK Aids" juu ya kushirikiana katika mapambano dhidi ya Dawa za Kulevya. Shirika la UK Border Force linaendelea kushirikiana kwa karibu sana na Jeshi la Polisi katika kudhibiti usafirishaji wa dawa za kulevya kupitia Uwanja wa ndege wa Zanzibar. Vile vile, maafisa wawili wa Kitengo cha Polisi cha Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar wameshiriki mafunzo ya udhibiti wa Dawa za Kulevya nchini Botswana (ILEA) kwa udhamini wa taasisi hiyo hiyo (Drug Enforcement Administration).

# 5.0 MAFANIKIO, CHANGAMOTO, HATUA ZA BAADAE NA HITIMISHO

## 5.1 Mafanikio

**Mheshimiwa Spika,** naomba sasa niyapitie mafanikio ambayo yamepatikana katika jitihada za kupambana na dawa za kulevya katika nchi yetu:-

i. Kuifanyia marekebisho makubwa *Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya Nam.9 ya mwaka 2009.*
ii. Kupunguza usambazaji wa dawa za kulevya kwa kukamata viwango vikubwa vya dawa za kulevya kabla ya kuwafikia watumiaji. Hii imetokana na kuimarika kwa mashirikiano ya kitaifa, kikanda na kimataifa ambayo yamepelekea kukua kwa mawasiliano.

iii. Serikali kupitia Tume imefanikiwa kutoa mafunzo ya *Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya* na marekebisho yake katika ngazi zote kuanzia Taifa, Mikoa, Wilaya, Shehia hadi ngazi ya Familia.
iv. Kusambaratisha na kuvunja maduka makubwa ambayo yalitumika kwa uhalifu huu wa dawa za kulevya.
v. Kuendeleza hatua za ujenzi wa kituo cha tiba na marekebisho ya tabia Kidimni kwa; maumbo ya ghorofa ya kwanza na ya pili ya jengo kuu, kuezeka pamoja na kukamilisha ununuzi wa vifaa kwa ajili ya kuendeshea kituo hicho.
vi. Kushiriki kikamilifu katika mikutano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ambayo imesaidia kukuza mashirikiano na mawasiliano na taasisi mbalimbali zenye kupambana za dawa za kulevya duniani.
vii. Kupunguza unyanyapaa kwa walioacha kutumia Dawa za Kulevya hivyo kuwasaidia watumiaji hao kupata huduma muhimu.
viii. Kuongezeka kwa vijana walioachana na Matumizi ya Dawa za Kulevya Zanzibar.

5.2 **Changamoto**

Changamoto zinazokabili juhudi za kupambana na dawa za kulevya ni:-

i. Jiografia ya nchi yetu inayoruhusu uwepo wa bandari nyingi zisizo rasmi (zaidi ya 271 Unguja na Pemba) ambapo ikizingatiwa kuwa kuna uhafifu wa vifaa vya ulinzi na utambuzi vya kutosheleza maeneo yote ya Visiwa;
ii. Ukosefu wa vifaa na utaalamu unaohitajika katika udhibiti wa usafirishaji wa dawa za kulevya katika mipaka yetu;
iii. Kuenea kwa matumizi ya rushwa katika kesi za kupambana na dawa za kulevya;
iv. Udhaifu katika taaluma ya kushughulikia masuala ya uhalifu wa dawa za kulevya;
v. Taasisi iliyopo sasa haina uwezo wa kisheria wa kuchunguza, kukamata, kupeleleza na kupeleka kesi mahkamani.

### 5.3 Hatua za Baadae

Serikali Kupitia Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya imepanga kutekeleza kazi zifuatazo katika harakati za kufanikisha mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

i. Kukifanya chombo cha udhibiti wa dawa za kulevya kuwa Mamlaka;
ii. Kuimarisha na kuendeleza kituo cha pamoja cha uendeshaji wa kesi za dawa za kulevya kwa kukamilisha muongozo wa uendeshaji wa kituo hicho (One Stop Centre);
iii. Kuendelea kuziwezesha Programu za Upataji Nafuu na kuendesha Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia kilichopo Kidimni;
iv. Kuwajengea uwezo wafanyakazi ili kuimarisha utendaji wa kazi kuendana sambamba na kasi ya mapambano ya dhidi ya dawa za kulevya;
v. Kuimarisha mahusiano na taasisi nyengine za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa katika udhibiti wa dawa za kulevya; na
vi. Kujenga Kituo cha Tiba na Marekebisho ya tabia kwa waathirika wa dawa za kulevya za kulevya Pemba kama ilivyoelekezwa katika Ibara ya 196 ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020 – 2025.

**HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi,**

Nawaomba muipokee, muijadili taarifa hii na kutoa mapendekezo yatakayoiwezesha Serikali kufikia lengo la kuifanya Zanzibar isiyo na matumizi ya dawa za kulevya.

Naomba kutoa hoja.

……………………………………………

**Dkt. SAADA MKUYA SALUM**
**WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS ZANZIBAR**